

Masuala ya Muungano: Maoni ya wananchi kuhusu nini kinachoendelea Zanzibar


Zanzibar ilikumbwa na matukio mengi wakati wa uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba 2015. Matokeo ya uchaguzi yalifutwa, huku Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ikisema kulikuwa na “ukiukwaji wa sheria ya uchaguzi”, na kupanga uchaguzi mpya kufanyika Machi 2016. Maamuzi hayo yalipingwa vikali na viongozi pamoja na wafuasi wa vyama vya upinzani na waliamua kutoshiriki kwenye uchaguzi huo mpya. Matokeo yake, Rais aliyekuwepo madarakani Dk Ali Mohamed Shein wa Chama cha Mapinduzi alishinda uchaguzi huo.

Je, wananchi wa Tanzania Bara wana mtazamo gani juu ya kile kinachoendelea Zanzibar? Je, ni kwa kiasi gani wanafahamu matukio yanayotokea Zanzibar? Na je, wana mtazamo gani kuhusu hatua zilizochukuliwa na serikali pamoja na vyama vya upinzani?


Takwimu za muhtasari huu zinatokana na utafiti wa *Sauti za Wananchi* iliyopo Twaweza. *Sauti za Wananchi* ni utafiti wenye uwakilishi wa kitaifa unaotumia simu za mkononi. Utafiti huu una uwakilishi wa Tanzania Bara. Taarifa kuhusu mbinu za utafiti zinapatikana kupitia www.twaweza.org/sauti. Takwimu za muhtasari huu zilikusanywa kutoka kwa wahojiwa 1,815 kutoka kundi la pili. Hii ikiwa ni awamu ya tisa ya kupiga simu kwenye kundi jipya, simu zilipigwa kati ya tarehe 29 Machi na 12 Aprili 2016.

Nusu ya wananchi wote (53%) hawafahamu matukio yanayotokea Zanzibar

Kielelezo cha 1: Je, unaweza kunieleza nini kimetoka Zanzibar tangu kufanyika kwa uchaguzi mkuu wa mwisho?



Wananchi 6 kati ya 10 wanakubaliana na ufutwaji wa matokeo ya uchaguzi mkuu (59%) na uamuzi



Chanzo cha Takwimu: *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 9 (Mei 2016)

Wananchi 4 kati ya 10 wanasema mshindi wa uchaguzi wa marudio atambulike kama mshindi halali

Kielelezo cha 3: kwa mtazamo wako ni njia ipi sahihi ya kushughulikia mgogoro wa kisiasa wa Zanzibar?

